



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

WARAKA WA SPIKA NA. 2/2020

KUHUSU

**MWONGOZO WA NJIA ZITAKAZOTUMIWA NA BUNGE KATIKA
KUJIKINGA NA MAAMBUKIZI YA UGONJWA WA CORONA**

MACHI, 2020

WARAKA WA SPIKA NA. 2/2020

KUHUSU

MWONGOZO WA NJIA ZITAKAZOTUMIWA NA BUNGE KATIKA KUJIKINGA NA MAAMBUKIZI YA UGONJWA WA CORONA

Waraka huu unarejea Waraka wa Spika Na. 1 uliotolewa kwa Waheshimiwa Wabunge, Wafanyakazi wa Bunge na Wadau mbalimbali wanaohusika na Shughuli za Bunge tarehe 16 Machi, 2020.

Ugonjwa wa Corona umeshathibitika kuingia hapa Nchini Tanzania na Serikali imeshatoa maelekezo ya kujikinga kupata na kueneza virusi vya Ugonjwa huo na pamoja na kueleza hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Wananchi wote katika kujikinga na Ugonjwa huo hatari.

Kwa kuzingatia msisitizo ambao Serikali imeutoa, sisi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa ni Taasisi inayohusisha wadau wengi tunao wajibu wa kuchukua ili kujikinga na vihatarishi vinavyoweza kusababisha au kuchochea Maambukizi ya Ugonjwa wa Corona. Kwa sababu hiyo, naleta Waraka huu unaotoa miongozo tunayopaswa kuifuata ili kujikinga na Ugonjwa wa Corona kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Vifaa vya kupimia joto la mwili (*thermo scanner*) na vya kuoshea Mikono (*Hand sanitizers*) katika Maeneo ya Bunge

Tumefanya utaratibu wa kupima joto la mwili kwa wote wanaoingia kwenye eneo la Bunge kwa kuweka vifaa vya kupima joto la mwili (*thermo scanner*). Aidha, katika kuhakikisha kuwa mikono yetu inakuwa safi na salama wakati wote, Ofisi ya Bunge imeandaa na kuweka vifaa vya kuoshea Mikono (*Hand sanitizers*) katika maeneo mbalimbali ya Bunge kama vile magetini, milangoni na kwenye mashine za *biometric*. Natoa wito kwa kila mmoja wetu kutumia vifaa hivyo kwa ufanisi kila wakati.

(b) Ziara za Kikazi za Kamati ndani ya Nchi

Ziara za Kikazi za Kamati zinazofanyika sasa zitaendelea hadi hapo itakapoamuliwa vinginevyo. Aidha, Kamati zinashauriwa kutotembelea maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu.

(c) Vikao vya Kamati

Vikao vyote vya Kamati vitafanyika kwenye Kumbi zilizopo katika maeneo ya Bunge. Aidha, Vikao vya Kamati vihusishe wadau wachache wanaohusika moja kwa moja na Hoja inayojadiliwa.

(d) Vikao vya Bunge

Vikao vya Mkutano wa 19 wa Bunge utakaoanza tarehe 31/3/2020 vitafanyika kama ilivyopangwa isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo.

(e) Safari za Kikazi nje ya Nchi

Safari zote za Kikazi nje ya Nchi zinasitishwa kwa muda hadi hapo itakapoamuliwa vinginevyo. Hii inahusisha ushiriki wa Bunge kwenye Vikao na Mikutano mbalimbali ya Kibunge. Kwa safari binafsi za Wabunge, tunashauri tahadhari ichukuliwe kujizuia kusafiri kwa sasa.

(f) Safari za Matibabu nje ya Nchi

Safari za Matibabu nje ya Nchi (kwa wanaogharamiwa na Bunge) hasa kwenye Nchi ambazo ugonjwa huo umesambaa zitasitishwa kwa muda na Vibali vya safari hizo havitatolewa hadi Serikali itakaposhauri vinginevyo.

(g) Semina na Mafunzo kwa Wabunge

Semina au Mafunzo yoyote yanayowahusu Wabunge yatatolewa katika Maeneo na Kumbi za Bunge tu.

(h) Wageni Bungeni

Utaratibu wa kupokea Wageni wengi ikiwemo makundi ya Wanafunzi au Wananchi wanaotembelea Bunge kwa lengo la kuona au kujifunza Shughuli za Bunge utasitishwa kwa muda hadi hapo itakapoamuliwa vinginevyo. Wageni watakaoruhusiwa kuingia Bungeni ni wale wenye kazi au shida mahsusi.

(i) Safari zilizofanyika hivi Punde

Kwa Wabunge au Watumishi wa Bunge waliotoka katika safari za nje ya nchi, watahitajika kupitia katika Zahanati ya Bunge kujiridhisha kama wapo salama kabla ya kuendelea na Majukumu yao ya kila siku Bungeni.

(j) Tahadhari nyingine za Kiafya

Pamoja na Miongozo iliyotolewa hapo juu, kila mtu atahitajika kuchukua tahadhari muhimu za kiafya kila wakati ili kujikinga na maambukizi ya Ugonjwa wa Corona. Tahadhali hizo ni pamoja na kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuepuka kusalimiana kwa kupeana mikono;
- (ii) Kutojichanganya kwenye watu endapo utajisikia kuwa na dalili zozote za Ugonjwa wa Corona;
- (iii) Kupata ushauri/msaada wa kitabibu kutoka katika Zahanati ya Bunge mapema endapo kuna dalili zisizokuwa za kawaida; na
- (iv) Kuziba pua na mdomo wakati wa kukohoa kwa kutumia vitambaa safi.

Natumaini Miongozo iliyofafanuliwa kwenye Waraka huu itasaidia kwa kiasi kikubwa katika kujikinga na maambukizi ya Ugonjwa hatari wa Corona. Tukizingatia mambo yaliyoelezwa hapa tutaisaidia Taasisi ya Bunge na Taifa kwa ujumla kuendelea kuwa eneo salama dhidi ya Ugonjwa huu ambao umeshatangazwa na Shirika la Afya Duniani kuwa ni Janga.

Waraka huu utatumika hadi hapo utakapotolewa Waraka au Maelekezo mengine.

Imetolewa na: Ofisi ya Spika,

S.L.P 941,

DODOMA.

17 Machi, 2020.